Kama uko tayari kutubu, kumpokea na kumfuata Yesu Kristo ili uweze kuenda mbinguni ukifa. Unaweza ukatumia ombi hili kumpokea Yesu Kristo sasa hivi:

''Baba yetu wa mbinguni, naja kwa msalaba na ufufuo wa Yesu . nimetenda dhambi, natubu na kuacha dhambi zangu. Kwa imani kupitia neema, nampokea Yesu Kristo kama bwana na mwokozi wangu . ingia moyoni mwangu Yesu, ninapofanya kukupenda, kukufuata na kukutumikia. Katika jina la Yesu , Amina.''

Tafadhali fungua ukurasa kusikia mengi kuhusu ulichokifanya kwa kumpokea Yesu Kristo kama bwana na mwokozi wako.

Pongezi! Kama ulimaanisha ombi, dhambi zako zimesamehewa na una uzima wa milele kupitia kwa Yesu Kristo! Bibilia inasema , '' ninawaandikia mambo haya ninyi mlioamini jina la mwana wa Mungu kusudi mjue kuwa mnao uzima wa milele'' (1 Yohana 5:13)

Lakini huu ni mwanzo tu kwako! Anza kukua kiroho kupitia njia zifuatazo:

**1. Masomo ya bibilia.** Anza na Yohana. **2. Omba kila siku,** ongea na Mungu na umskize. 3. Kanisa. Fuata kanisa ambayo inafunza bibilia na inaamini Yesu Kristo alikua Mungu katika utu. 4. Waeleze wengine jinsi umempokea Yesu Kristo leo na jinsi wao wanaweza kumpokea!

Tafadhali wasiliana na huduma yetu na utuambie umempokea Yesu Kristo na tunaweza kukupa hatua zitakazofuata na vifaa vya kukukuza kiroho!

**Scott Nute Global Ministries**
**info@scottnute.org - www.scottnute.org**
**Houston, Texas, USA**



## JE, NIKUULIZE?

Ukifa leo una **uhakika 100%** utaenda mbingunu?

Hivi ndivyo utakavyo hakikisha

Mungu anakupenda na anataaka uwe naye maishani sasa na hata milele mbinguni baadaye. *'nami nimekupenda' (Isaya 43:4)*



Dhambi inatutenganisha na upendo wa mungu.

Bibilia inasema, *''wote wametenda dhambi''* (Warumi 3:23). Dhambi zetu zatuelekeza mautini,hukumunu na jehanamu, ambavyo sivyo Mungu atakavyo.



Yesu kristo, kifo chake msalabani na kufufuka kwake kwamaanishankwamba Yesu Kristo alikua Mungu katika utu na ndiye njia pekee ya dhambi zetu kusamehewa. Yesu alisema,'' *mimi ndiye njia na kweli na uzima, mtu hawezi kufika kwa baba bila kupitia kwangu. (Yohana 14:6)*

**Uamuzi ni wetu.** Ni sisi wenyewe kuchagua tutakachofanya na Yesu Kristo, kumkubali au kumkataa. Sasa tutaamua kama tutaenda mbinguni au jehanamu baada ya kufa kulingana na tutakachofanya na Yesu Kristo. Uamuzi wako ni upi kumhusu Yesu?

**Amwaminiye yeye hahukumiwi;** asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakumwamini mwana pekee wa Mungu. (yohana 3:18)



Unapaswa kufanya nini kuwa na uhakika100% utaenda mbinguni?



1. **Tubu:** Twafaa kuacha dhambi na ni Mungu tu anayeweza kufanya hivi. Ni kama kugeuza mwenendo na kuachaa kuacha kutawala maisha yetu na kumruhusu Yesu Kristo atawale. *“kwa hiyo tubunimumgeukie Mungu ili azifute dhambi zenu'' (matendo ya mitume 3:19)*

2. **Pokea.** Kwa imani tunafungua mioyo yetu na kupitia kwa neemaya Munguwala sio kwa matendo yetu mazuri au nguvu zetu,tunapokea Yesu Kristo kama bwana na mwokozi..... ni kama kupokea zawadi ya bure.

   *“bali wote waliompokea na kumwamini aliwapa haki ya kufanywa wana wa Mungu” (Yohana 1:12)*

3. **Fuata.** Kama ushahidi kuwa tumetubu na kumpokea Yesu Kristo, tunaanza kumfuata. Hii yamaanisha, matendo yetu, maneno na maisha yetu yanaanza kubadilika. Yesu alisema, *''njooni mnifuate na nitawafanya wavuvi wa watu'' (Mathayo 4:19)*